



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI  
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



## TAARIFA KWA UMMA

### MAKAO MAKUU YA LATRA KUHAMIA DODOMA KUANZIA 26 SEPTEMBER 2022

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inautangazia Umma kuwa Makao Makuu yake yatahamia Dodoma kuanzia **Jumatatu tarehe 26 Septemba, 2022**. Hatua hii ni utekelezaji wa Agizo la Serikali kwa Wizara na Taasisi zake kuhamia Makao Makuu ya Nchi Dodoma.

Ofisi za Makao Makuu Dodoma zitakuwa katika Jengo la LATRA lililopo kwenye Kiwanja Na. 6 Kitalu "A" eneo la NCC Nyuma ya Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete Barabara ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na baina ya majengo ya Ofisi za Takwimu (NBS) na Mkandarasi (CRB). Hivyo, kuanzia tarehe 26 Septemba, 2022, mawasiliano yote na LATRA Makao Makuu yatakuwa kwa anwani ifuatayo:

**Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA),  
S.L.P. 1742,  
41104 Tambukareli,  
DODOMA, TANZANIA.  
Simu +255 262 323 930  
Barua pepe: [dg@latra.go.tz](mailto:dg@latra.go.tz) , [info@latra.go.tz](mailto:info@latra.go.tz)**

Aidha, Huduma za LATRA zitaendelea kutolewa katika Ofisi za Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara.

**Imetolewa na:  
Kitengo cha Mawasiliano  
16 Septemba, 2022**